

Uhuru na Amani

GAZETI LA KANISA LA KINJILI LA KILUTHERI TANZANIA TOLEO LA 2, 2014 Bei Sh. 500



Vol. 114, Toleo la 2, 2014



ISSN 0856 - 1214

Upendo FM 107.7



Amani kwa wote

JE UNAFAHAMU KITUO BORA CHA REDIO KATIKATI YA JIJI?

Kwa matangazo ya biashara na mikutano ya Injili,
kwa ushauri wa kiroho na maendeleo ya jamii:
Tangaza kwenye Redio bora ya Upendo na Amani
kwa wote.

Fika sasa LUTHER HOUSE
GHOROFA YA PILI
SOKOINE DRIVE.

Upendo FM 107.7 Mhz
P.O. Box 13603
Da es Salaam, Tanzania

Simu: 022 212 4228/ 2139556/ 2124221

E-mail: upendofm@yahoo.com

Radio Furaha 96.7 FM

Sikiliza matangazo ya
kituo bora cha Redio Iringa
na maeneo jirani.

Kwa maoni, ushauri wa kiroho
na kijamii wasiliana na:

Meneja: Protas Kanemela
Simu: +26 27 003 43

Fax: +255 262 701 198

Barua pepe: elctrdrd1987@yahoo.com

Wakala

Gazeti la Uhuru na Amani
Unapolipa kwa TT NBC; tafadhalili
tuma kivuli cha Pay-in-Slip kwa
Mhariri kwa njia ya Barua Pepe:

<elobulu@elct.or.tz>

A/C ni ile ile: Na: 014103002064



Ifahamu RADIO SAUTI YA INJILI

FM 92.2 & 96.2 MHz
MOSHI

RSYI ni rafiki anayekujali kiroho na kimwili.
Katika Masafa ya FM, Radio Sauti ya Injili
kutoka Moshi inasikika vizuri kabisa katika
Masafa yafuatayo:

Moshi	92.2 MHz	Mlalo (Lushoto)	102.6 MHz
Arusha	96.2 MHz	Kisosora (Tanga)	96.7 MHz
Same	100.4 MHz	Morogoro	96.6 MHz
Kibaya (Kiteto)	102.9 MHz	Hakwe (Rombo)	96.4 MHz

Aidha Radio Sauti ya Injili, Moshi inasikika kwenye tovuti
dunia nzima kwa saa 24 www.sautiyainjili.org

Radio Sauti ya Injili inatangaza vipindi
mbalimbali vikiwemo vya maendeleo, afya,
uchumi, habari na halikadhalika vipindi vya
mafundisho ya dini. Unaweza kupata habari
moto moto za kitaifa na kimataifa katika kipindi
cha Dira ya Leo.

Wasiliana na:
Mkurugenzi RSYI
S.L.P. 777, Moshi

Simu: 027 27 52772 au 027 27 53080

E-mail: redio@elct.org

Tovuti: www.sautiyainjili.org

Kumbuka kuwa RSYI ipo kwa ajili yako. Aidha, kijamii.
Endelea kuimarisha huduma nzuri hii kwa hali na mali.



Uhuru na Amani ni Gazeti la Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT). Hutayarishwa na Kitengo cha Mawasiliano, KKKT.

Maoni yaliyomo katika makala zinazochapishwa ni ya mwandishi anayehusika na wala hayawakilishi mawazo ya Kanisa ama mhariri isipokuwa pale ambapo imetamkwa wazi.

Ukiwa na maoni, ushauri, makala au maswali mwandikie:

Mhariri
Uhuru na Amani
S.L.P. 3033
ARUSHA

Barua pepe: elobulu@elct.or.tz
 sms kwa Mhariri: 0754-482-285

Fungua Tovuti ya KKKT:
<http://www.elct.org/>

MHARIRI **Elizabeth Lobulu**

Limepigwa Chapa na:
Moshi Lutheran Printing Press
 S.I.P 301 Moshi
lutheranpress@yahoo.com

Newspaper Design & Typesetting:
Elizabeth Lobulu

Wachangiaji wa Makala:
 Mch. Dkt. Faith Lugazia
 Askofu Dkt. B. K. Bagonza
 Mallumbo W. Mallumbo
 Askofu Mteule A. Mwaipopo
 Mary Joel Mmbaga
 Mch. Naibu Nyambo
 Mch. Anza Amen Lema
 Agnes Amos
 Mch. Charles Mzinga
 Mch. Emmanuel Simbo
 Mulashani Haveson

PICHA YA JALADA:
Wajumbe wa Mkutano Mkuu
wa 16 wa Wanawake KKKT
wakijiandaa kuandamana.

PICHA: © 2014 GAZETI LA UPENDO / EMMANUEL KIMWERI

MAONI YA MHARIRI

Ni muafaka kuombea amani

Tanzania inasifika kwa kuwa kisiwa cha amani na kwa hilo inatupasa watu wote kuwa macho kubaini na kuzuia watu wanaotaka kuifanya nchi isiwe na amani.

Mchungaji mmoja hivi karibuni alipokuwa akifundisha Somo la Biblia kuhusu maonyo ya kupenda pesa aliwaliza waliokusanyika: Je, ungependelea nini katika familia zaidi ya chochote. Mmoja alisema angependa awe na pesa maana zinakuwezesha kufanya kila kitu.

Lakini kadiri alivyouliza wengine wakasema ni kweli fedha itakupa mahitaji muhimu; lakini kikubwa katika familia fedha hizo zikupe amani. Baadhi walitoa mifano kuwa fedha zimewahangaisha watu wakazitumia vibaya kwa anasa za kidunia. Hivyo mfundisha somo alihitimisha kwa kusema tafuteni kuwa na amani na watu wote ndipo mengine yote yatafuata.

Na Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) alipokuwa akifundisha Somo la Biblia kuhusu umoja katika Mkutano Mkuu wa Dayosisi ya Kaskazini Kati akinukuu Yohana 17:21 inayosisitiza kuwa ‘wote wawe na umoja’. Na alibainisha mambo ambayo yakiwepo inaonekana kwamba kuna umoja mahali husika. Alisema umoja ni matokeo ya: upendo, kusikilizana, kuchukuliana mizigo, kuheshimiana, kusamehe na kusahau. Kwa maneno rahisi Mkuu pia alikuwa anazungumzia amani.

Alisema kuwa sheria inayotawala ulimwengu ni ya kulipizana visasi. Kwa mfano vita vilivyopo barani Afrika na hata Mashariki ya Kati chanzo chake ni kulipizana kisasi. Akatoa mfano kwamba hata watoto wadogo wanapocheza mitaani mmoja akipigwa ngumi na mwenzake mara moja na mwenzake atalipiza. Hivyo alisema viongozi wasiwe watu wa kutaka kulipizana visasi bali ni bora kujua yanayopaswa kutenda ikitokea shida (1Nyakati 12:32). Nukuu hiyo inahusu wana wa Isakari, watu wenye akili za kujua nyakati na yawapasayo kutenda. (Soma zaidi andiko hilo uk. 17 wa toleo hili).

Mgogoro ukitokea ni gharama kubwa kurekebisha mambo yarudie hali ya kawaida. Kwanza muda mwingi unapotea na pili kujenga mahusiano na vitu vilivyoharibika au vilivyo simama kwa sababu za migogoro pia inagharimu nguvu na mali nyingi.

Ni heri kuzuia kwa kufanya majadiliano na maelewano kuliko kusubiri hali ichafuke sana. Na sasa tunapoelekea kwenye mchakato wa Uchaguzi Mkuu wa 2015 tuombe sana Mungu asaidie nchi yetu iwe na amani kipindi chote hiki na hata baada ya uchaguzi. Mungu atuwezeshe Watanzania tuendelee kuwa na uzalendo na amani itawale kila jambo na si kutaka kulipizana kisasi. Neno la Mungu linatuagiza ‘pendanieni’. Hivyo tuoneshe upendo hata kwa maadui zetu ambao nao wana haki ya kusikilizwa, kuchukuliwa mizigo, kuheshimiwa na kusamehewa. Ee Mungu Ibariki Tanzania Yetu.

Msiwarubuni wananchi - Pinda



Waziri Mkuu, Mhe. Mizengo Peter Pinda (Kushoto), alipomkabidhi zawadi Askofu Amoni Mwenda baada ya kuingizwa kazini ili kuongoza Dayosisi ya Ruvuma huku Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Alex Malasusa, akishuhudia (kulia).

Viongozi wawe na hofu ya Mungu

Mamia ya wakazi na wageni wa mji wa Songea walijitokeza kwa wingi 27 Julai 2014 katika Ibada ya kuwekwa wakfu na kuingizwa kazini Askofu Amon Joel Mwenda kuongoza Dayosisi mpya ya 23 ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT). Ibada hiyo pia ilikuwa na tendo la kuzindua rasmi Dayosisi ya Ruvuma.

Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Alex Malasusa, katika Mahubiri yake alisema, Kanisa lingependa kupata viongozi wacha Mungu. "Inashangaza baadhi ya watu wanagombea nafasi za uongozi lakini hawana hofu ya Mungu wala upendo kwa watu anaotaka kuwaongoza.

"Bila kujali imani ya mtu, tunatamani tungepata kiongozi anaye mcha Mungu, anayependa kuhudhuria Ibada na kumpenda Mungu ndipo atawapenda watu anaowaongoza," alisitiza.

Kipaumbele ni elimu na Afya

Akitoa hotuba yake ya kwanza mara baada ya kuingizwa kazini, Askofu Mwenda,

alisema Dayosisi itashirikiana na Serikali na wadau wa ndani na nje katika kutoa huduma za kijamii hasa elimu na afya na kuhimiza ufanyakazi za kilimo ili wakazi wake wawe na akiba ya kutosha ya chakula.

Alisema "Dayosisi mpya ya Ruvuma imezaliwa katika kipindi chenye changamoto nydingi za kidunia na utandawazi, ukiwemo mmomonyoko mkubwa wa maadili.

"Mbali ya kufundisha Neno la Mungu, tutakabiliana na changamoto za mmomonyoko wa maadili, rushwa, mauaji ya albino, unajisi wa watoto na ubakaji wa wanawake." Alisema.

Dayosisi hiyo mpya iko katika Mkao wote wa Ruvuma na Wilaya ya Ludewa - eneo ambalo lina ukubwa wa kilometra za mraba 72,630. Kati ya hizo km. za mraba 64,233 ni za mkoa wa Ruvuma.

Epukeni kugeuzwa mtaji

Waziri Mkuu, Mhe. Mizengo Pinda ambaye alihudhuria Ibada hiyo, aliwaonya Watanzania wawe makini na viongozi wanaopenda kutoa rushwa hasa katika kipindi

cha kuelekea Uchaguzi Mkuu wa 2015. "Kama mtu ana nia ya kweli ya kuongoza ni kwa nini atumie fedha ili kupata nafasi ya uongozi?" Alihoji.

Alitaka wananchi kuwa makini na wasije wakageuzwa mtaji wa kuwanufaisha watu binafsi.

"Tukikubali kutumika ni sawa tutapata viongozi wakati wa uchaguzi; lakini watakuwa ni wale wasio na hofu ya Mungu, wenye kujali maslahi yao kuliko ya wananchi waliowachagua," aliongeza.

Aliwaomba viongozi wote wa dini pamoja na waumini wote waendelee kuliombea Taifa ili Mungu aliepushe na janga hilo la watu kupenda rushwa. Alitumia fursa hiyo pia kuhamasisha wazidi kuuombea mchakato wa kupata Katiba Mpya ili Wabunge wote warejee Bungeni na kuikamilisha kazi waliyoianza.

Alimwomba Askofu Mwenda apookee jukumu hilo kwa mikono miwili na kuahidi kuwa Serikali itakuwa naye bega kwa bega kuwaongoza Watanzania walioko kwenye Dayosisi ya Ruvuma.

Huruma kwa jirani ni wajibu wa Kanisa



**Na Mallumbo W. Mallumbo,
Naibu Katibu Mkuu Mipango na
Maendeleo KKKT.**

Mvua zilizonesha mwishoni mwa mwezi Aprili 2014 zilisababisha mafuriko makubwa katika Tarafa mbili za Wilaya ya Kyela (Unyakyusa na Tenende).

Baadhi ya wananchi walijaribu kuyakimbia mafuriko kwa kutumia daraja bovu. Inaaminika watu saba walipoteza maisha kwa jinsi hiyo.

Mwezi Juni 2014 kwa njia ya ACT Alliance (Shirika la Kimataifa la Makanisa la misaada ya dharura),

Endelea uk. 6

Baadhi ya wananchi wa kijiji cha ltope wakijaribu kuyahama makazi yao.

(Picha: © 2014 KKKT/ MALLUMBO W. MALLUMBO)



Gari la Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Mhe. Abbas Kandoro (kushoto), alipokuwa akijaribu kuwafikia wananchi waliokumbwa na maafa ya mafuriko Wilayani Kyela.



Mawasiliano kati ya Wilaya ya Kyela na vijiji vya ltope, Mpunguti, Nyerere, nk. yalikatika kwa muda na kufanya wananchi wategemee daraja la miguu kama linavyoonekana pichani ambapo walikuwa na wakati mgumu kwa kuwa lilikuwa limeharibika.

Mwakilishi ACT Alliance ashuhudia ugawaji

Inatoka uk. 5

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) lilipata USD 35,000 sawa na Tsh. 56,000,000 kuwasaidia waliopata maafa haya.

Licha ya matatizo yaliyojitekeza wakati wa kuanza kazi hii tunamshukuru Mungu kwani baada ya mahojiano/vikao katika ngazi mbalimbali; milango ya kuwahudumia waathirika hao ilifunguliwa.

Kwa kufuata barua ya Mkuu wa Wilaya kwa Waziri Mkuu na kwa jamii yenye Kumb. Namba AB,117/124/01/76 ya 24/4/2014 watu 18,976 walihitaji



msaada wa kijamii.

Hesabu hii ilikuwa kubwa kuliko uwezo, hivyo KKKT ilikubaliana na viongozi wa Wilaya kuhudumia watu 3,400 tu kwa kuwapatia kila mmoja wao kilo 10 za mahindi na kilo 20 za maharagwe kwa kila Kaya ambapo kaya zisizopungua 601 zilipata huduma hii.

Ikiwa ni sehemu ya Uinjilisti katika zoezi la usambazaji wa chakula hicho, ofisi ya wafadhili (ACT Alliance) kutoka nchini Uswisi (Switzerland) iliwasilishwa na Mratibu wa Kitengo cha Maafa Barani Afrika (isipokuwa Afrika ya Kusini) na Asia, Bi Florine Jobin, ambaye ziara hii ilikuwa ya kwanza kwake kuikanyaga ardhi ya Afrika Mashariki.

Bw. Mallumbo aliwakilisha KKKT na Bi Jobin alitoka ACT Alliance.



Daraja la mbao ambalo hutumika kuvuka kwa miguu nalo lilikuwa limeharibika kama linavyoonekana.

Inaendelea uk. 15



Ugawaji wa chakula cha msaada kwa waliokumbwa na mafuriko Wilayani Kyela 2014. PICA: © 2014 ACT ALLIANCE/ FLORINE JOBIN

Tafakari kuhusu ‘Uhuru wa Mkristo’ na ‘Matengenezo’ eneo la Afrika Mashariki

Na Mchg. Dkt. Faith K. Lugazia
Mhadhiri, Chuo Kikuu cha Kiprotestanti, Butare-Rwanda

Makala hii fupi, haitazami sana katika mafafanuzi ya Martin Luther, bali itajikita kwa wakati wetu Karne ya 21. Mwandishi atatoa uzoefu na kutafakari kuhusu ‘**kuwekwa huru**’ kama inavyojitekeza katika makundi ya Karismatiki hapa Afrika Mashariki; na kuwa tunaposherehekeea ‘**Matengenezo ya Kanisa**’ tufanyeje?

UTANGULIZI:

Chimbuko la ‘**Uhuru wa Mkristo**’ ni Waraka wa Mtume Paulo **IKor 9:19** ambapo Martin Luther alilitumia kuweka sawa uelewa wa fundisho hili kwa uongozi wa Kirumi, Kanisa, na baadhi ya makundi ya uamsho.

Makundi hayo yalidai kuwa **Kristo akituweka huru** basi Roho Mtakatifu humfundisha na kumuelekeza muumini juu ya imani na maadili mema ndani ya jamii, na hivyo Kanisa na Sakramenti zake havina maana wala nafasi kwa muumini.

Luther alikataa mafundisho hayo kwa kusema kuwa ingawa ‘Mkristo ni kiumbe huru’ na si mtumwa wa yeyote, bado Mkristo huyo huyo ni mtumishi na ‘**mtumwa wa wote**’. Maana yake ni kuwa ingawa tumewekwa huru, mbali na dhambi kwa neema; uhuru wetu bado una mipaka, inayotutaka sisi kuwa watumishi wa Kristo na watumishi wa wengine. Ukombozi wa Kristo unatuelekeza kumpenda Mungu na kufanya matendo ya upendo kwa jirani.

Makala hii fupi, haitazami sana katika mafafanuzi ya Martin Luther, bali itajikita kwa wakati wetu Karne ya 21. Ni maoni ya mwandishi kwa uzoefu wake kuhusu makundi ya Karismatiki, tafakari za kuwekwa huru kwa makundi ya Karismatiki hapa Afrika Mashariki. Hivyo tunapoendea sherehe za miaka 500 **Matengenezo ya Kanisa** 2017 tufanyeje?

Kundi la kipentekoste hapa Afrika Mashariki ni kubwa kuliko kundi lolote la Ukristo. Wanachama wa kundi hili ndani ya makanisa ya kimission hujulikana kama wana karismatiki. Ndani ya makanisa ya Kipentekoste yenyе utaratibu wa uongozi, hujiona

kama makundi ya uamsho. Wanachama wake wengine ni vikundi vya huduma na makanisa ambayo yanaitwa ya Upentekoste wa kileo.

Niseme makundi haya yamekuwa huru kweli kweli ndani ya Yesu Kristo



Mchg. Dkt. Faith K. Lugazia.

kwa sababu: **Kwanza**, yamekataa kuwa chini ya uongozi wa kimagharibi kama yalivyoanzishwa wakati wa makanisa ya kimissioni. Wala hayako chini ya makanisa yaliyoanzishwa na Waafrika. Makundi haya yanadai kuanzishwa na Roho Mtakatifu wa Mungu kwa kuwafunulia viongozi wake kufanya huduma ya umisioni.

Pili, makundi haya yameamua kujisomea na kufanua Biblia kutoka katika ufhamu wao kama Waafrika. Na kuangalia Biblia inavyoweza kujibu mahitaji ya maisha yao pasipo kuingia katika mafafanuzi na tafakari na hivyo mara nyingi kufanya ujumbe ukubalike kwa wateja wake. Mfano mmoja wa mafundisho yake ni kuwa ukiwa na hitaji ukaomba kwa kufunga, jinsi unavyoongeza muda wa kufunga na kuomba ndivyo Mungu anavyokusikia

na kukutimizia mahitaji yako. Ama mtu anaweza kutoa fungu fulani la pesa na kumpa mtumishi wa Mungu akaomba kwa ajili yake na Mungu akatenda.

Si hilo tu lakini kuna fundisho lingine kwa mtazamo mwandishi linatisha zaidi. Fundisho la unabii kwa kutumia ufhamu wa Kiafrika. Baadhi ya manabii hao wanadai kuwa na uwezo wa kuona mtu aliyesababisha matatizo muumini aliyonayo. Kwetu Tanzania kuna mahusiano yaliyovunjika kati ya wazazi na watoto ama wana familia sababu ndani ya makundi hayo, manabii wameonyeshwa ama kaka, dada, mama au mama mkwe kuwa ndiyo sababu ya mwanakundi kuwa mgumba, kuugua, nk.

Hii inatisha sababu Kristo aliyejua kutupatanisha anapowaacha waumini wake katika kufarakana, swali je, Kristo alikuja kufanya nini? Linakosa jibu lake. Mafundisho ya kundi hili kwa ujumla ni matokeo ya utandawazi ambapo yanachukua mchanganyiko wa mafundisho ya utamaduni wa Mwfrika, na ya utamaduni wa kimagharibi na kufanya yaenee ndani ya mafundisho ya Biblia.

Nionavyo uhuru wao umevuka mipaka kwani sasa baadhi ya waumini ndani ya makundi haya wamekuwa na uhuru hata wa ama kumweka Mungu ndani ya mifuko yao na kumfanya Mungu kama roboti ambaye wanaweza kumuita ama kumwambia chochote watakacho na wakati watakao. Aidha wameonesha Mungu kwa sura yake moja tu, kwamba kule kuwa ndani ya Yesu, maisha ni raha na amani pasipo mateso ama kuubeba msalaba.

Kanisa letu wala Kanisa lolote si kipimo cha kuwataka kundi hili waamini tunavyofikiri ama kupenda. Na tena ni makosa tukiwahukumu kwa kipimo cha mafundisho ya urithi wetu. Katika hili, nionavyo mimi, tunaposherehekeea miaka 500 ya **Matengenezo ya Kanisa** turudi tena katika kuleta umoja. Kwa kutekeleza hili Kanisa letu lifanye juhudii za kipekee katika kuwa na midahalo na mijadala na makundi haya katika kurudi kwenye ukweli wa Neno la Mungu. Kwamba **kuwekwa huru** si kumfanya Kristo kuwa mtumwa wako kwa kufanya kila kitu muumini apendacho bali ni kuwa na mipaka inayotutaka badala yake kuona uhuru wetu katika pande zake mbili na yote yakiongozwa na **neema ya Kristo tu**. <flugazia001@luthersem.edu>

Ni Massangwa Kaskazini Kati



Mch. Solomon Jacob Massangwa (wa pili kushoto) alichaguliwa na Mkutano Mkuu wa 23 wa KKKT Dayosisi ya Kaskazini Kati kuwa Askofu na Mch. Gideon Paulo Kivuyo (wa pili kulia) amechaguliwa kuwa Msaidizi wa Askofu. Mkutano huo ulifanyika 21 - 25 Julai katika Shule ya Sekondari Peace House ya jijini Arusha. Mkuu wa KKKT Askofu Dkt. Alex Malasusa (kushoto) alifundisha Somo la Biblia na kusitiza umoja. Soma zaidi uk. wa 17. Kulia ni Mch. Joel Nangole ambaye ni Mwenyekiti wa Katiba wa Dayosisi ya Kaskazini Kati.



Askofu Amon Kinyunyu wa KKKT Dayosisi ya Dodoma akimzika. Mch. Sara Oforo aliyekuwa Katibu wa Idara ya Wanawake wa Dayosisi tangu Feb. 2010. Askofu alimshukuru Mungu kwa utumishi wa Mch. Oforo aliye fariki 8 Agosti 2014. Alisema pamoja na mambo mengi Mch. Oforo aliye kuwa mwanzilishi wa 'lbada ya Nyumba kwa Nyumba'.

Watumishi wamaliza mikataba, waagwa


Baadhi ya watumishi wa Ofisi Kuu ya KKKT waliomaliza mikataba yao hivi karibuni na kuagwa rasmi, mionganoni mwao ni hawa katika picha:



Bibi Byera Hermn,
LMC.



Dkt. John Hilary,
Kitengo cha Afya - Utetezi.



Bibi Kristin Pors,
DanMission.



Mch. Anicet Maganya,
Kitengo cha Utetezi.

Chuo cha Ualimu Makete

Na Mch. Naibu Nyambo

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Kusini Magharibi, lipo katika mchakato wa ujenzi wa Chuo cha Ualimu eneo la Itamba.

Uwekaji wa jiwe la msingi wa chuo ulifanyika 06/07/2014 ultanguliwa na Ibada iliyofanyika katika Kanisa Kuu Magoye na kuongozwa na Baba Askofu Job T. Mbwiyo akisaidiwa na Msaidizi wa Askofu Mch. A. Ngavo.

Jiwe la Msingi liliwekwa na Msaidizi wa Askofu toka Sinodi ya Carolina ya Kusini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Marekani

akisaidiana na Baba Askofu Mbwiyo.

Chuo hicho kitakacho julikana kwa jina la 'Trinity' kikamilika kitatoa ajira kwa jamii, sambamba na kupata watalamu wa kada mbalimbali. Kwa sasa chuo kipo katika hatua ya ujenzi wa madarasa na maabara.

Waliohudhuria siku hiyo ni pamoja na Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, Mhe. Dk. Binilith S. Mahenge ambaye ni Mbunge wa Makete.

Katika salamu zake alishukuru KKKT kwa kuona umuhimu wa kuwa na chuo cha Ualimu Wilayani

Makete. Alisema "chuo hiki si kwa ajili tu ya wanamatamba ni cha jamii nzima ya Kitanzania na pengine hata nchi za nje.

"Huu ni wakati wa Sayansi na Teknolojia, vijana wetu wanapaswa kuingia huko kwa kuijandaa vyema kielimu.

"Kanisa mmeliona hilo kwa niaba ya Serikali napenda kulishukuru Kanisa kwa kuona umuhimu wake. Hii ni kwa sababu, kumpa mtu elimu huo ndio ukombozi wa kudumu kifikira.

"Chuo hiki kitakuwa ni chachu ya kuleta ukombozi huo," alisema na alishukuru pia Kanisa la Marekani

kwa mchango wao katika sekta ya elimu, maji, sare za wanafunzi, ujenzi wa nyumba za yatima, nk., katika shule mbalimbali katika eneo la Matamba.

Sherehe hizo pia zilizohudhuriwa na wadau wengine wa ujenzi wa chuo hicho kutoka Mbeya na Iringa. Kwaya ya Tumaini Matamba, UKWATA Itamba zilitumbuiza.

Mwisho Askofu Mbwiyo aliwashukuru wadau kwa kutoa michango yao na aliwataka kuendelea kutoa nguvu zao kwa hali na mali kwani kazi bado ni kubwa katika ujenzi huo.

Mkutano Mkuu wa Vijana 2014

NENO KUU: “*Mkiukomboa wakati maana zamani hizi ni za uovu,*” Efeso 5: 16

Viongozi waaswa wasiwe madikteta



Askofu Mteule Solomon Massangwa, KKKT Dayosisi ya Kaskazini Kat.

Mkutano Mkuu wa Pili wa Vijana KKKT ulifunguliwa 10 Julai 2014 kwa Ibada ilioongozwa na Kaimu Mkuu wa Dayosisi ya Kaskazini Kat, Mchg. Solomon Massangwa, (Askofu Mteule) kwa Neno toka Waefeso 5: 17.

Alisema Kanisa la Bwana huanzia nyumbani mahali kijana alipo, iwe chumbani au mahali popote. Lakini pia Kanisa huanzia kwenye familia za baba na mama na hii inasaidia kumwandaa kijana asipende mambo ya peke yake ili atakapokwenda kuhudumia nje asiwe na utawala wa imla (dikteta).

Alisema uongozi wa imla unaweza kutumika pale ambapo uharibifu unaweza kujitokeza wakati ushawishi umeshindikana, ila alisisitiza kwamba kwa kawaida kiongozi lazima atumie njia ya ushawishi ili kufikia mafanikio.

Mwisho alisema kuwa uovu utaondoshwa wakiwemo viongozi wanaomcha Mungu na wanaolewa tulipo na tunapoelekea. Alisisitiza hayo kwa kunukuu toka: Mwa 2: 15; Mwa 2: 17, Mwa 3: 9, Mdo 9: 1; Yoh 2: 14 na Rum 12: 2.

Wakati ni kipawa kutoka kwa Mungu. Kijana inampasa atumie wakati vizuri kwa kuijelimisha, kuondokana na umaskini, kuitumikia jamii na kumwabudu Mungu.

Vijana wafundishwe Neno la Mungu waweze kumfahamu Mungu na mapenzi yake ili wapate maarifa ya kuepuka uovu na kutumia muda wao wa ujana vizuri. “*Jinsi gani kijana aisafishe njia yake, kwa kutii na kulifuata Neno la Mungu...Moyoni mwangu nimeliweka Neno lako nisije nikakutenda dhambi,*” (Zab 119: 9, 11).

Vijana wawe na ratiba ya majukumu yao ya kila siku. Wafanye mambo yaliyo sahihi, mahali sahihi na kwa wakati sahihi maadamu wao ni watu sahihi (kazi na sala). Viongozi na walezi waliopata semina katika Mkutano Mkuu wa Pili wa Vijana, wawe mfano wa kuigwa kwa wengine. Vijana wahusiane na makundi yenye maadili

Askofu Mteule Ambele Mwaipopo, Dayosisi ya Ziwa Tanganyika, alifundisha Somo la Biblia katika Mkutano Mkuu wa Pili wa Vijana.



Askofu Mteule Ambele Mwaipopo.

mazuri na yanayojenga kanissa na jamii kwani makundi mabaya huharibu tabia njema (*bad company corrupts good behavior*).

Kanisa na Dayosisi iwe na ubunifu wa njia nzuri za kuwavuta vijana kama michezo, vikundi vya ujasiriamali, ziara, majadiliano, nk. Pia ufuutilaji wa kundi la vijana uwe ni wa karibu sana kwani yako mambo mengi yanayowavuta

vijana hasa katika ulimwengu huu wa utandawazi.

Vipindi vya kujifunza Biblia na dini vitiliwe mkazo katika shule za msingi, sekondari na vyuo ili kuwajengea msingi mzuri wa maadili mema.

Wazazi na walezi waone wajibu wao kufundisha watoto katika familia zao ili wakue katika msingi mzuri kama Neno la Mungu linavyohimiza.

Kanisa litumie vyombo vya habari vya Kanisa na vya Dayosisi zake kama redio, tovuti, majarida na magazeti kutoa elimu za maadili kwa vijana.


Wachungaji walio waratibu na makatibu wa vijana katika Dayosisi za Kanisa wapeleke ujumbe huu kwa Wachungaji wenzao katika Dayosisi zao ili wawe na umoja na ushirikiano katika katika kulea kundi la vijana.



Baadhi ya wajumbe wa Mkutano wa Pili wa Vijana walipokuwa wakijitambulisha. PICA: © 2014 KKKT/ MADUKA MADUKA

Kijana mkristo katika utumishi

Mada kuhusu Kijana Mkristo na Utumishi iliwasilishwa na Askofu Dkt. Paulo Akyoo wa KKKT Dayosisi ya Meru (pichani chini), ambaye alisema kijana Mkristo katika utumishi awe mbunifu, anayekubali kujitao kikamilifu ili kufikia malengo yake na mwenye moyo wa huruma; yaani ajali huduma



**Askofu Dkt. Paulo Akyoo, KKKT
Dayosisi ya Meru**

zaidi kuliko masilahi yake binafsi.

Askofu alisema kuwa umri wa vijana ni kati ya miaka 15 – 35. Alitaja kuwa vijana wana maono, na kwamba wale wasio na maono wasaidiwe wawe nayo.


Popote kijana alipo Ukristo wake uonekane - iwe ni mahali pa kazi ama popote atakapokuwepo - awe chumvi na nuru kwa watu wote katika kumuinua Kristo. Anatarajiwa awe mjasiriamali

anayefanya kazi yake kwa uaminifu akiwa na hofu ya Mungu na mwenye malengo ya kimaono kwa ajili ya kutimiza ndoto za maisha yake.

Kijana Mkristo ni mtu mbunifu wa kazi hivyo vijana waandaliiwe wajiajiri wenyewe. Alishauri kila Dayosisi ialike wataalamu wa ujasiriamali ili vijana wafundishwe. Aliuliza je, kijana Mkristo ni nani? Na alijibu kwa kuorodhesha vifungu vifuatavyo: 1Yoh 2:14; Zab 119: 9 -11; Efeso 6: 10 -12, 22; 1Timo4:12 na Ebr 10:23 -25.

Kanisa liwajibike kuona umuhimu wa kuwekeza nguvu zake kwa vijana, kwa kuwapa mafundisho sahihi juu ya ujana wao, jinsi ya kuenenda Kikristo, kumtegemea Mungu siku zote, ili mafundisho hayo yaweze kuleta matokeo chanya katika utumishi wao hapo badaye.

Alihimiza vijana watiwe moyo wasikate tamaa, wafundishwe wakae ndani ya Kristo, (Yoh 15: 4 -8) kwani nje ya Kristo ni mtumwa wa Shetani. Kijana asipotumiwa na Mungu atatumwa na dunia (Shetani). Kijana ndani ya Yesu ana uhuru, amani na anaweza kumtumikia Mungu. Vijana ni nguzo ya Kanisa hivyo katikati ya vijana tupate watu wenye fani mbalimbali na wazitumie fani hizo kwa ajili ya utukufu wa Mungu, alisema.



Vijana watakiwa kuwa chumvi

Katibu Mkuu wa KKKT, Bw. Brighton Killewa (pichani juu), amewaasa vijana kuwa **nuru na chumvi ya ulimwengu** wakati alipokuwa akitoa salamu katika Mkutano Mkuu wa Pili wa Vijana wa KKKT uliofanyika Olasiti Garden, jiji Arusha, 9 - 13 Julai 2014.

Alisema, KKKT imetoka kwenye Fungamano la Makanisa ya Kilitheri Tanganyika ambapo 19 Juni 1963, yaliungana na kuwa Kanisa moja lililoitwa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT). Hivyo, alisisitiza umoja uwepo kwenye uongozi wa vijana. Pia alinukuu maneno toka Mathayo 5: 13 - 16 na kusisitiza: "**Vijana ni chumvi na nuru ya ulimwengu.**" Aliwaasa vijana kuhakikisha kuwa wanaifahamu na kuitangaza Taswira na Dhamira ya Kanisa.

Arusha yawa mwenyeji Mkutano Mkuu wa Pili wa Vijana



Picha ya pamoja wakati wa Mkutano Mkuu wa Vijana KKKT uliofanyika Hotel ya Olasiti Garden, jiji Arusha 09 - 12 Julai 2014. Pamoja na mambo mengine walipokea na kujadili mada, ripoti mbalimbali na kuchagua wajumbe wa kamati mbalimbali.

Kijana atakomboaje wakati

Kijana Mkristo ni lazima ajitambue na kujiamini katika Kristo Yesu. Anaweza akawa ni kiongozi wa Idara ya Vijana Usharikani au Jimboni hivyo hana budi kumtumikia Mungu kwa moyo wake wote, nguvu zote na mali alizonazo kama kuijunga na kwaya au kufundisha Neno la Mungu kwenye semina za vijana au mikutano ya vijana.

Pia atumie nafasi kuhubiri Injili ya Yesu Kristo kanisani na kwenye mikusanyiko (mikutano) ya watu wa Mungu. Pia aeneze Injili kwa wakristo wote waliokufa (walioanguka) kiroho na wale wasiomjua Kristo kabisa.

Binafsi ninafanya ziara mbalimbali nje ya eneo langu kwa lengo la kueneza Injili ya Yesu Kristo kwa kuwa nampenda Yesu. Pamoja na kumtumikia Mungu kwa njia mbalimbali pia ni mjasiriamali mdogo katika eneo langu ninaloishi.

Nahakikisha shughuli hizi nafanya kwa uaminifu. Nashukuru Mungu kwamba shughuli ninazofanya ni za halali.

Baadhi ya changamoto za huduma kwa vijana ni pamoja na: Vijana wengi kutojitambua na kutojiamini; elimu ndogo hasa ya ujasiriamali; vijana kupenda sana anasa za dunia kiasi cha kutolitii Neno la Mungu. Changamoto nyingine ni ushirikiano mdogo kati ya viongozi wa Kanisa na Idara ya Vijana.

Pamoja na kumtumikia Mungu nakuendeshashughuli zangu za ujasiriamali wa kibashara pia ninajiedeleza kwa kujilipia masomo katika Chuo Kikuu Huria Tawi la Singida: Shahada ya Menejimenti ya Rasilimali Watu (Bachelor of Human Resources Management).

Namshukuru Mungu kwa



Agnes Masania Amos,
Dayosisi ya Kati.

kuniwezesha kumudu haya yote kwa pamoja na kunipa

mbinu za kuyafanikisha.

Ni muhimu sana kwa vijana kuukomboa wakati pale anapojitambua kuwa yeye ni nani na anatakiwa afanye nini na kwa wakati gani pasipo kuathiri jambo lingine muhimu. Na kwa kuwa vijana wengi hawajui namna ya kuukomboa wakati.

Hivyo nashauri Kanisa lifanye yafuatavyo: Elimu ya Kikristo itolewe kwa usahihi na kwa wakati kwa kuandaa semina na mikutano mbalimbali

MAONI YA WASHIRIKI

Kijana na utandawazi

Kanisa lishirikiane na taasisi nyingine za kiimani kutoa elimu kwa vijana kuhusu matumizi sahihi ya vyombo vyya mawasiliano kama redio, TV na intaneti kwa njia ya semina na vipeperushi na mashulen.

Wamiliki wa vyombo vyya mawasiliano waelezwe umuhimu wa kutoa kipaumbele kwenye matangazo katika vyombo hivyo kwa mtazamo wa kujenga jamii badala ya kujali biashara.

Kanisa na taasisi nyingine za kiimani likemee kwa nguvu zote vipindi au matangazo yote yanayoleta mmomonyoko wa maadili katika jamii.

Vijana wakubwa, wazazi na walezi wawe dira ya vijana wadogo kwa kutumia vyombo vyya mawasiliano kwa kuleta maendeleo na kutunza maadili ya jamii husika bila kujali wamesikia au wameona nini kwenye vyombo vyya mawasiliano.

Familia kama kanisa la



Na Emmanuel Simbo,
Dayosisi ya Dodoma.

kwanza (baba, mama na watoto) ione umuhimu wa kukaa pamoja kwa kushirikishana tarifa sahihi kwa uwazi (bila kificho) juu ya faida na hasara za vyombo vyya mawasiliano vilivyopo katika jamii.

Kanisa na Serikali kukaa pamoja ili kuandaa sheria ndogondogo za kuwabana wamiliki wa vyombo vyya mawasiliano kutorusha vipindi na matangazo yanayomomonyoa maadili ya jamii hasa nyakati za mchana.

Kwa maoni wasiliana na mwandishi kwa anwani: <Simboemma25@gmail.com>

sharikani na majimboni, ili vijana wajengewe uwezo wa kujiamini na kujitoa kumtumikia Mungu wao kwa uaminifu na usafi.

Inafaa vijana washawishiwe kwenda kusomea utumishi wa Mungu (Uchungaji na Uinjilisti) na wale wasio na uwezo kifedha wapewe ruzuku. Pia vijana wapewe elimu ya ujasiriamali ili wawewe kujiajiri.


Kwa maoni wasiliana na mwandishi kwa anwani: <agnesnasania@yahoo.com>

Ujasiriamali ni muhimu


Ni muhimu na ni wakati muafaka kwa Kanisa kuwa na mipango na mikakati ya makusudi kuendesha mafunzo na pia kuwawezesha vijana kuweza kujitegemea wenye kwa ujasiriamali kwa kuwapa mitaji kwa njia ya mikopo ya mzunguko ili vijana wengi wawee kubadilika katika mipango endelevu ya kuwawezesha vijana kiuchumi.

Wasaidiwe kuona fursa zilizopo katika maeneo yao mfano fursa za ardhi, elimu, mikopo, biashara, n.k. Pia vijana wawe na utayari wa kujifunza na kuona fursa mbadala na kuzitendea kazi kwa uaminifu.

Kwa maoni wasiliana na mwandishi kwa anwani: <semzinga@yahoo.co.uk>



Mch. Charles Mzinga,
Dayosisi ya Mashariki na Pwani.



Mulashani Haveson, Makamu Mwenyekiti.

Vijana wasiige maadili potofu

Tabia ya baadhi ya vijana kuiga mambo katika dini/madhehebu mengine ni ya mtu binafsi na msimamo wake juu ya Mungu wetu. Wale wanaoiga mambo katika mitandao kuhusu sayansi na teknolojia ni suala zuri la maendeleo katika jamii na Kanisa kwa jumla. Ila inategemea: je, teknolojia hiyo unaitumiaje katika kielimisha jamii na wewe binafsi.

Urithi wa mafundisho ya Kilutheri unaboreshw na maendeleo ya sayansi na teknolojia tuliyonayo kwa sasa. Kwa mfano uimbaji kwa kutumia vyombo vya muziki vya kisasa. Mungu azidi kutupigania katika kudumisha mila na desturi ya Kanisa letu la Kilutheri.

Kwa maoni wasiliana na mwandishi kwa anwani: <mhaveson@yahoo.com>

Uchaguzi wa wanakamati




Baadhi ya wajumbe wa Kamati ya Utezi wakihesabu kura.

Akitoa mada: **"Kijana Mkristo na Changamoto za Utandawazi na Uchumi,"** Injinia Tunzo Mzava ambaye ni Mhadhiri toka Kitengo cha Biashara Chuo Kikuu cha Mt. Meru jijini Arusha alisema, ni muhimu vijana wabuni miradi mbalimbali ili kukua kiuchumi na kuacha utegemezi na hiyo kupata nafasi ya kuimariika kiimani

Mratibu ahimiza umoja

Mratibu wa Dawati la Vijana KKKT, Mchg. Anza Amen Lema, amehimiza vijana kuwa na umoja ndani ya Kanisa. "Suala la umoja ni msingi wetu unaotokana na Neno la Mungu, katika kushirikishana vipawa na karama kwa faida ya wote," Alisema hayo wakati akiwasilisha ripoti yake mbele ya Mkutano Mkuu wa Vijana KKKT kwa kuongozwa na Neno la Mungu toka Yoh 17: 21. Alisema wimbi la mafundisho potofu ambapo baadhi ya vijana wameathiriwa na mafundisho hayo ni moja ya changamoto za Kanisa kwa sasa. Aliomba Dawati lipatiwe chombo madhubuti cha usafiri ili kuwaunganisha vijana. <anzalema@elct.or.tz>



Mchg. Anza Amen Lema.

Kijana Mkristo na Utandawazi

Na Injinia Tunzo Mzava

pia.

Miradi itasaidia vijana watoke kwenye kundi la watu waliokosa ajira ambalo ni sawa na kuwafanya wawe ni watumwa wa wengine.

Katika utangulizi wake Injinia Mzava alizungumzia utandawazi katika Kanisa na si upande wa kijana tu. Alisema utandawazi ni kama 'kamba tatu zinazofunga dunia iwe tandawazi' ambazo ni: **uchumi**, jamii na siasa. Utandawazi umefanya 'dunia kuwa kijiji'. Teknolojia na sayansi imefanya dunia ikawa ndogo sana. Dunia kuwa kijiji inasaidia Kanisa kuhubiri Injili kirahisi.

Alisema teknolojia itumike kuhubiri Injili, kwa mfano Ukristo ulisambazwa kwa

nguvu kupitia mawasiliano, mageuzi ya kisiasa na mateso. Aliongeza kuwa kila wakati kulipotokea mabadiliko duniani, Roho Mtakatifu ametumia njia hizo kueneza Ufalme wa Mungu.

Alishauri Kanisa liuone utandawazi katika njia sahihi (chanya) ikitumika katika njia sahihi. Alisema kwa upande mwingine Shetani naye hajalala, watumishi wa shetani wanafanya kazi kama vichaa, wakati watumishi wengi wa Mungu wanafanya kazi kwa udhaifu.

Aliulizamaswali yafuatayo: Ni watumishi wangapi wa Mungu wameweza kuwekeza kupitia utandawazi? Tunaposema **ufalme wako uje** nani atakuwa wakala



Lightness Moses Kisaka,
Dayosisi ya Mbulu.

Vijana wasidharauliwe

Na Lightness Moses Kisaka

Kijana anatakiwa ajiamini katika kile anachokifanya na chenyе kumpendeza Mungu. Hivyo atumie utandawazi kumhubiri Mungu kwa vijana wenzake huku akikomboa wakati na kuaminika na jamii anayoihudumia. Vijana wasikubali mtu ye yote kuudharau ujana wake bali atumie vipawa aliyopewa na Mungu kuitangaza ukristo bila kuona haya. Atoe huduma za kijamii bila ubaguzi, upendeleo au kujali maslahi binafsi.

Kijana asive tegemezi bali awe mwenye kuwashawishi vijana wenzake kuwa ni kipi wanawenza kufanya ili kujikomboa kiuchumi bila kutegemea njia zisizo halali katika kutafuta riziki. "Na hata sasa najua ya kuwa yoyote mtakayo mwomba Mungu, Mungu atawapa," Yoh 11: 22. Tudumu katika maombi katika kila jambo. sms: 0786 361 936

wa huo ufalme? Je, kuna TV ngapi za Walutheri? Radio na hata Magazeti? Kuna majukwaa kupitia utandawazi, tumeyatumia kiasi gani?

Ingefaa taasisi zote zitoe elimu kwa vijana juu ya matumizi sahihi ya utandawazi kama kompyuta, barua pepe, intaneti au mitandao ya kijamii ili kijana mkristo asione dhambi juu ya matumizi ya teknolojia hiyo, (Mithali 4:13).

Vile vile hata viongozi wajifunze kutumia teknolojia ili kuweza kuongoza vizuri vijana walioko kwenye utandawazi, 1Timoteo 4:13.

Kijana ahamashishe kuwa mbunifu kwa kufikiri mambo makubwa ili kuleta mabadiliko yake, katika Kanisa na jamii kwa ujumla.

Kwa maoni wasiliana na mwandishi kwa anwani: <mzavatunzo@yahoo.co.uk>

Mkuu ataka wazazi kukemea uovu



Mkuu wa KKKT Askofu Dkt. Alex Malasusa akizindua Bweni la Wasichana, Shule ya Sekondari Mkusa, Kibaha kabla ya kuongoza Ibada ya kufungua Mkutano Mkuu wa 16 wa Wanawake KKKT.

Mkuu wa KKKT Askofu Dkt. Alex Malasusa aliwataka wanawake kuhakikisha wanawakemea vijana wanapotenda maovu.

“Zamani watu wazima walichapa watoto wakikosa, siku hizi mambo haya yameachwa. Wanawake rudisheni hali hiyo na kusimama katika nafasi kwa kusema ukweli juu ya vijana wa sasa wanaopotea,” alieleza Askofu.

Akifungua Mkutano Mkuu wa 16 wa Wanawake KKKT uliofanyika Kibaha 8 - 12 Julai 2014, alihoji kuwa

Kanisa litakuwa na faida gani kama haliwezi kukemea vijana huku akisisitiza umuhimu wa wanawake kuwasaidia vijana ambao wengi wao sasa wamekuwa walevi, watumiaji wa lugha za matusi na


Habari na picha: Emmanuel Kimweri/ Gazeti la Upendo.

kuvaa mavazi yasiyompendeza Mungu.

Alisema kazi hiyo inapaswa kufanywa na wanawake: “Saidieni familia bila kujali ni ya kwako au jirani kwa kuwa



1



2



3

1. Wajumbe wakiwa katika Ibada ya ufunguzi wa Mkutano wa 16 wa Wanawake KKKT.
2. Mchg. Rachel Axwesso alifundisha Somo la Biblia: Isaya 7:4.
3. Mkutano Mkuu wa Wanawake ulifanya maandamano; ulipokea na kujadili mada, ripoti mbalimali na kufanya uchaguzi wa viongozi.
4. Mkutano ulimchagua Mwenyekiti mpya wa Wanawake, Bibi Mary Laiser, toka KKKT Dayosisi ya



Kaskazini Kati kuchukua nafasi ya Bibi Monica Ngavatula toka KKKT Dayosisi ya Kusini.

vijana wanapotea,” aliongeza Askofu.

Alisema mafundisho potofu yameenea na mawindo rahisi ni wanawake. Hivyo, aliwataka kusimama imara na kutegemeza imani zao katika kulikuza Kanisa la Mungu na jamii kwa ujumla.

Aidha, Askofu Malasusa baada ya kupokea maandamano ya wajumbe wa Mkutano huo alifungua Bweni la Wasichana la Shule ya Sekondari ya Wasichana Mkusa (mahali mkutano huo ulikofanyikia). Shule hiyo inayomilikiwa na Wanawake KKKT Dayosisi Mashariki na Pwani.

Askofu Malasusa alisisitiza wanawake kuendelea kutambua nafasi zao katika Kanisa kwa kushiriki kuanzisha miradi mbalimbali ya kuisaidia jamii.

Alitoa rai kwa Dayosisi za KKKT pamoja na madhehebu mengine kuendelea kuwatumia wanawake katika ngazi mbalimbali za maamuzi kutokana na uwezo wao mkubwa wa utendaji katika kazi za Kanisa.

Mkuu atoa gari kwa Kurugenzi ya Wanawake

Baada ya ibada, risala zilitolewa ndipo Mkuu alitoa gari lake aina ya Toyota Land Cruiser litumike kufanya kazi za wanawake. hatua iliyofanya wajumbe kusimama na kulipuka kwa nderemo na vifijo.

Tulianza vibaya Tumalize vizuri - Askofu Bagonza

Na Askofu Dkt. Benson K. Bagonza

Kama tulivyoona katika toleo lililopita la **Uhuru na Amani**, mchakato wa kuandika Katiba hapa nchini, ulianza vibaya na ulijaa kasoro kadhaa zilizobainishwa katika makala hiyo. Wakati naandika makala ile, Bunge Maalum la kuandika Katiba Mpya lilikuwa linaendelea mjini Dodoma. Haikuchukua muda mrefu, Bunge hilo liliarishwa kwa madai ya kupisha Bunge la Bajeti.


Lakini wiki chache kabla ya kuahirishwa, wabunge karibu wote kutoka vyama vya upinzani vyenye wabunge pamoja na wajumbe kutoka kundi la 201, walisusia na kutoka nje ya bunge hilo. Kundi hili kwa sasa linatambulika kama UKAWA, yaani "Umoja wa Katiba ya Wananchi".

Kundi la UKAWA limesusia vikao vya Bunge maalum kwa madai makubwa



Askofu Dkt. Benson K. Bagonza,
KKKT Dayosisi ya Karagwe.

mawili. **Kwanza**, wanadai kuwa Chama tawala (CCM) kwa kutumia wingi wa wabunge wake, kinapuuza maoni ya wananchi yaliyomo ndani ya rasimu ilioletwa mbele ya Bunge na Jaji Joseph Warioba. **Pili**, wanadai wabunge




Askofu Dkt. Owdenburg Mdegella,
KKKT Dayosisi ya Iringa.

Bunge la Katiba lifutwe

Askofu Owdenburg Mdegella wa KKKT Dayosisi ya Iringa ameungana na baadhi ya watu wanaopendekeza Rais Jakaya Mrisho Kikwete wa Tanzania afute Bunge la Katiba kwani linapokutana bila maridhiano toka makundi ya pande zote halitakuwa na mafanikio bali ni kupoteza bure fedha za walipa kodi.

Spika atakubali mabadiliko ya rasimu



Mhe. Samwel Sitta,
Mwenyekiti wa Bunge Maalumu la Katiba.

Mwenyekiti wa Bunge Maalumu la Katiba Tanzania, Mhe. Samwel Sitta, anaona ni heri Bunge lifanyike kwani uandikaji Katiba ni jambo la ushawishi na kuelewana na maelewano hayo yatawezekana Bungeni.

Kuhusu hoja ya kufanya marekebisho mapendekezo ya Katiba Mpya badala ya kujadili ilivyo ili hatimaye kuikubali au kuiakataa. Mwenyekiti huyo amesema wajumbe wana uhuru wa kubadili jambo linaloonekana libadilishwe.

'Hainingii akilini watu 600 kujadili rasimu na kuifanya uhariri mdogo mdogo kisha kukubaliana nayo ilivyo,' alisema.

wa CCM wanatumia lugha za matusi na ubaguzi dhidi ya wapinzani.

Wanaweka sharti kuwa ili warejee bungeni, CCM wakubali kujadili rasimu iliyowasilishwa na Tume ya Warioba pia CCM waache kutumia matusi na lugha za ubaguzi dhidi ya wajumbe wenye maoni tofauti na wao. Mpaka hapa, mchakato wa katiba mpya umekwama. Nini kifanyike ili kunusuru mchakato huu?

Kiini cha mgogoro ni muundo wa Serikali ya Muungano. Wakati CCM wanataka muundo wa serikali mbili, tume ya Warioba imependekeza muundo wa serikali tatu. CCM wanadai serikali tatu ni maoni ya tume, si maoni ya wananchi na tume inadai haya ni maoni ya wananchi. Inahitajika hekima na uzalendo kuokoa mchakato huu. Nionavyo mimi, yanahitajika mambo makuu matatu kwa pande zote.

Kwanza, UKAWA watambue kuwa hawajaisusia CCM bali wamewasusa wananchi waliowatuma bungeni kuwawakilisha. Wakati huo huo, CCM watambue kuwa hata kama wamebaki ndani ya jengo lakini wamesusa maoni ya wananchi kwa kung'ang'ania muundo ambao haukupendekezwa na tume.

Pili, muundo wa serikali ndiyo roho ya serikali. Mambo mengine yote katika katiba hujengwa katika muundo. Kwa hiyo, UKAWA na CCM watambue kuwa wanacheza na roho ya serikali.

Tatu, maridhiano ndiyo msingi mkuu wa kuandika katiba yoyote. Maridhiano hayategemei wingi wa wajumbe walio kila upande bali hutegemea uungwana wa kukubali kupoteza kitu fulani na kupata kitu fulani (*give and take*).

Ili kuondoka katika mkwamo huu, anahitajika mtu wa katikati anayeweza kuwaambia UKAWA mambo wasiyopenda kusikia, lakini pia mtu huyo awaambie CCM mambo ambayo kwa kawaida hawakuzoea kuyasikia. Hapa inahitajika taasisi, mtu binafsi au kundi.

Kwa bahati mbaya, taasisi na makundi mbalimbali ya ndani ya nchi, yameisha jichanganya kwa kuwa yana wajumbe ndani ya Bunge Maalum la Katiba. Maandiko Matakatifu yanashuhudia kuwa katika hali kama hii, ndipo alihitajika nabii wa kusema kwa niaba ya Mungu mwenyewe.

Kanisa liko bega kwa bega na Serikali



Baadhi ya watu waliovuka mto kukimbia mafuriko wakitafakari
hatua ya kuchukua baada ya kuvuka mto.

Inatoka uk. 6

Jobin alishiriki katika vikao kadhaa katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kyela. Tunamshukuru Mungu kuona kwamba mamlaka zilizopo Wilayani Kyela ziliidhinisha Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania ligawanye msaada huo kwa wananchi walioathirika na baa la mafuriko.

Pamoja na kutoa misaada wakati wa maafa, KKKT ni mdau wa maendeleo na lipo bega kwa bega na Serikali katika kutimiza azma yake ya kuhudumia jamii. KKKT hutoa asilimia 15 ya huduma ya afya nchini kupitia mahospitali, vituo vya afya na zahanati zilizotapaka

maeneo mbalimbali nchi nzima.

Bwana wetu Yesu Kristo kadri tunavyomsoma katika Maandiko Matakatifu tunabaini ya kwamba alijaa huruma, alikuwa mtumishi wa watu, alizifahamu haja za watu waliomzunguka na alikuwa faraja ya wengi (Lk. 4:18, 4: 12-13, 8: 26 – 56, Yh. 12: 32-35, Mt. 15:32-35). Pamoja na kuwa faraja kwa wengi, analiagiza Kanisa ambalo ni mimi na wewe ku wahudumia wengine.

“Kwa maana nalikuwa na njaa, mkanipa chakula; nalikuwa na kiu, mkaninywesha; nalikuwa mgeni, mkanikaribisha; nalikuwa uchi,

mkanivika; nalikuwa mgonjwa, mkaja kunitazama; nalikuwa kifungoni, mkanijia” (Mt. 25: 35 – 36).

Katika vipaumbele vya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania; kipaumbele cha kwanza ni huduma za kiroho hasa uinjilisti na cha pili ni Diakonia. Hivyo kuliona Kanisa likijihuisha na kuhudumia waliokumbwa na maafa aidha yaliyosababishwa na watu wengine kama vile: vita, uhreibifu wa mazingira na ama maafa ya asili kama vile mfumuko wa tetemeko la ardi haitakuwa ajabu kwa sababu linastahili kuwa hivyo.

Kanisa lisilowajali wahitaji litakuwa sawa na mikusanyiko ya wachawi ambao siku zote nia yao ni kuwaangamiza au kuona wengine wakiangamia aidha kwa kukosa maarifa au kwa kusababishiwa na wengine. Heri yule/wale ambao watakapokutana na Bwana Yesu wataweza kumuuliza maswali yafuatayo:

“Bwana, ni lini tulipokuona una njaa, tukakulisha, au una kiu tukakunywesha? Tena ni lini tulipokuona u mgeni, tukakukaribisha, au u uchi, tukakuvika? ni lini tena tulipokuona u mgonjwa, au kifungoni, tukakujia”? (Mt. 25: 37c – 39).



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Abbas Kandoro akiongea na wananchi.

Mchg Maumbuka kuongoza mradi wa nishati jadidifu

Mchg. Thomas Efraim Maumbuka amejiunga na programu ya Uhai na Mazingira ili kuongoza Kitengo cha Nishati Jadidifu, Ofisi Kuu ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) kuanzia Juni Mosi, 2014.


Kabla ya kujiunga na Ofisi Kuu ya KKKT, Mchungaji Maumbuka alikuwa Naibu Katibu Mkuu Mipango na Maendeleo KKKT Dayosisi ya Kati 2005 - Mei 2014.

Alizaliwa 12 Juni 1974 mjini Singida na alipata mafunzo ya Cheti cha Injinia Ujenzi toka Chuo cha Ufundii Misungwi Wilayani, Mwanza alikosoma 1997 hadi 1998. Na mwaka 2000 - 2004 alichukua

mafunzo ya Uchungaji na kutunukiwa Stashahada ya Theolojia ya Chuo cha Kilutheri Kiomboi, Singida.

Alibarikiwa kuwa Mchungaji tarehe 06 Februari 2005 katika Usharika Mkuu wa Immanuel, Singida Mjini.

Alifanya kazi ya Uchungaji katika Sharika mbalimbali za Dayosisi ya Kati ikiwa ni pamoja na Usharika wa Ngimu 2004 – Julai 2005; Mwankoko 2012 - Nov. 2012; Mgori Desemba 2012 - Julai 2013 na Usharika wa Manyoni Agosti 2013 - Mei 2014. Mchg. Maumbuka ameoana na Rosemary Masangwila na kwa pamoja wamejaliwa watoto wawili -wa kiume na wa kike.



Mchg. Thomas Efraim Maumbuka.

Ifahamu Program ya KKKT ya Huduma ya Afya ya Msingi

Zifuatazo ni picha kuonesha baadhi ya huduma zinazofanywa na Program ya Afya ya Msingi (HAM) ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania.



Gari la Wagonjwa kwa wanawake wajawazito mali ya Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe: Ni mkakati mmoja wapo kupunguza vifo vya wanawake vijijini. Pikipiki hutumika kukokota gari hilo.



Timu ya HAM ilikutana na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Morogoro Vijijini kushawishi ili Zahanati ya Mkulazi iweze kuingia mkataba wa huduma na Serikali.



Mtoto asiyiona Shuleni Irente / Rainbow Dayosisi ya Kaskazini Mashariki: Watoto hawa wanahitaji vifaa maalumu vya kujifunza na walimu wao nao wanahitaji nyenzo maalumu za kufundishia.



Uvunaji wa maji ya mvua kwa matumizi ya Zahanati ya Mkulanzi inayokabiliwa na tatizo la maji.

Picha: (c) 2012 PROGRAM YA HAM KKKT/
RICHARD MWAKATUNDU

Wana Dayosisi lindeni umoja- Mkuu

Na Askofu Dkt. Alex Malasusa,
Mkuu wa KKKT

Kichwa cha Mkutano Mkuu wa 23 wa KKKT Dayosisi ya Kaskazini Kat 2014 kilikuwa: "**Wote wawe na umoja**," Yoh 17: 21.

Umoja ni jambo la ndani wala si jambo la kushinikizwa au la kusema tu bali ni la vitendo kutokana na mtu anavyojojisikia ndani na ndipo wengine wataona kwamba kuna umoja.

Kichwa hiki hakikuchaguliwa kwa bahati mbaya bali mazingira ya ufarakano kabla na baada ya kifo cha Askofu Dkt. Thomas Laiser (aliyefariki 7 Feb 2013); yalihitaji umoja katika Dayosisi.

Kipindi hicho tunawenza kusema umoja ulikuwa mahututi na baada ya wana dayosisi kudumu katika maombi, Mungu amerejesha Dayosisi yake katika umoja (makofi na vigelegele).

Katika umoja tunapatana na kukubaliana kuwa kitu kimoja. Viongozi wanapata wenyewe kwa wenyewe na Washarika wanapata na viongozi wao ili wote wawe wamoja na kusameheana; **ya kale yamepita nasi tunakuwa viumbe vipyä!**

Katika 1Nyakati 12: 32 tunasoma wana wa Isakari **walijua nyakati na yawapasayo kutenda**.

Wakati huu Kanisa linahitajika katika jamiili na ndilo liwezalo kukemea rushwa na kutojipendelea lakini kama Neno lisemavyo, **lazima kwanza wawepo watu wenyе akili**, ili kusimamia haya. Ni wakati Kanisa linatakila kusimamia umoja katika taifa hili na hatuwezi kufanya hivyo kama sisi hatuna. Ni lazima sisi wenyewe tukae pamoja ndipo tuweze kuombea taifa umoja.

Wazee muwaonye vijana wasichezee mambo ya Kanisa na tuhimize usomaji wa Biblia. Baadhi yetu tumeshuhudia wale wanaosumbua Kanisa wakipatilizwa hadi wajukuu zao. Tunapaswa kupinga na kukemea roho zinazotesa Kanisa. Yoh 17: 1 – 21 ambayo ni sala ya kikuhan kuna mambo matatu yanahimizwa:

Kwanza, Yesu anajiombea mwenyewe (Yoh 17: 1 – 5). Nasi tujifunze kujiombea, kuombea familia na kutoa ushuhuda wetu binafsi.

Pili, aliwaombea wanafunzi (Yoh 17: 6 – 10) na sisi tujifunze kuombea wengine. **Tatu**, anawaombea watu wa mataifa (Yoh 17: 20 – 26) ikiwa ni hata sisi KKKT na Dayosisi ya Kaskazini Kat; tulioimbewa na Yesu katika sala hii nzuri ya Kikuhani.

Yesu aliona nini hadi afanye maombi hayo? Labda alipomwangalia Petro hakuangalia udhaifu bali matokeo mazuri baada ya Petro kuomba siku ya Pentekoste na Kanisa la kwanza kuzaliwa. Labda alimwangalia Yuda Iskarioti lakini hakuona udhaifu bali aliona umuhimu wa kuombea umoja wa wanafunzi. Aliye kinyume cha umoja ni Shetani hivyo matukio ya kupiga Wachungaji au kuharibu umoja ni ya Shetani.

Katika Dayosisi Mashariki na Pwani zilitokea faraka za kutaka kubaguana kikabila na hayo tulishinda kwa kulenga



Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Alex Malasusa, mara baada ya kupewa zawadi kwa kufundisha Somo la Biblia katika Mkutano Mkuu wa KKKT Dayosisi ya Kaskazini Kat. Kulia ni Askofu Mteule Solomon Massangwa na Msaidizi wa Askofu, Mchg. Gideon Kivuyo (katikati).

katika kushikamana na kujenga umoja imara zaidi kuliko mwanzo. Ninapo mtazama Mkristo, Mchungaji au Askofu sitazami kabilia lake na ninapoitwa katika huduma katika Dayosisi yoyote ile ya KKKT naona mtumishi ni ndugu katika Bwana; nami naingia katika kanisa popote naona fahari kutumika **Nyumbani kwa Bwana**, (vigelegele ana makofi). Hivi karibuni yupo msharika aliyetoa shukrani sh. milioni 100. Hata hapa, dayosisi ikiwa na umoja deni la dayosisi litilipika tu. Tusibaki kuangaliana kwa matabaka ya kikabila bali tushirikiane katika kila jambo ili kazi isonge mbele. Hata Yuda akiondoka atakuja Sauli na baadaye ataitwa Paulo **aliyemwinua Yesu**.

Yesu aliwaombea **wote wawe na umoja kama baba alivyo ndani yangu nami niwe ndani yao**. Mungu anataka tuone baraka zake tuwapo ndani ya umoja. Tutamani tuweze kuwa chachu ya kujaza umoja na watu wote **wajue ndiye uliyetutuma**. Inapasa Kanisa liwe na umoja ili kuwa tofauti na dunia. Kanisa ni zaidi ya NGO au taasisi za kidunia. **Kanisa la Mungu ni kundi la watakatifu**. Yapo makundi ya Shetani. Katika Ufunuo Yohani **anawaandikia watakatifu**.

Ili Kanisa lioneokane lazima umoja uwepo. Umoja ni matokeo ya: **Upendo unaonekana**; **Kusikilizana** kwa kukubaliana bila unafiki; **Kuchukuliana mizigo** kwa kutotangaza ubaya wa wengine ili asisamehewe. Matokeo mengine ya umoja ni **kuheshimiana**. Yaani viongozi kuheshimu walio chini na walio chini kuheshimu viongozi. Pia ni **kusamehe** na kusahau.

Mtu akishachaguliwa kuwa kiongozi hata kama amesoma na Msharika hana budi kuweka mipaka. Mfano ni chupa ya soda ambayo kitaalamu huachwa hewa kwa juu ili soda isioze. Vivyo hivyo viongozi waachiwe nafasi ya kuongoza vizuri na Washarika wawaheshimu viongozi kwa kutowaingilia eti kwa kuwa kwa ni kumoja au wamesoma wote. Mkifanya hivyo wote mtaozia, (kicheko na makofi).

Kwa kkuomba '**wote wawe na umoja**', inadhihirisha Yesu ametumwa

na Mungu. Huenda mambo mabaya yamepita ukatamani bora fulani afe. Neno linatukumbusha hata **kuwaza ni dhambi**. Tushukuru Mungu kwamba Yesu hakurudi jana na kama hujamsamehe mtu umembeba ndani yako "**achia**". Ombo msamaha maana Yesu anataka kutufundisha kusameheana.

Kuna nguvu inayopunguza kwa mtumishi aendaye kutumika madhababuni akiwa na mizigo. Musa aliambiwa na Mungu: "**Vua viatu vyako mahali unapokanya ni patakatifu**." Madhababu ni mahali patakataku tusepeleke mizigo.

Kanuni inayotawala ulimwenguni ni kulipizana kisasi. Iwe ni katika vita vya sasa vya Mashariki ya Kat 1 na kwingineko; ni hali ya kulipizana kisasi. Hata watoto wakicheza mitaani mmoja kipigwa ngumi na mwenzake atalipiza (kicheko). Lakini Yesu amesema **sisi si wa dunia hii**. Biblia inasema **kisasi ni cha Mungu**. Hivyo viongozi mnapofanya mabadiliko au mnapokuwa mnahudumia watu wasihihi kwamba mnalipiza kisasi.

Meli ikiingia katika maji ni sawa lakini maji yakiingia katika meli itazama. Kanisa kuwa ulimwenguni ni sawa lakini ulimwengu unapoingizwa Kanisani siyo sawa. Dalili zake ni kule kushindana, kuumizana, kukashifiana kwa barua za posta, barua pepe, mitandao ya kijamii, nk.

Dalili nyiningine ni kwa wale wanaotaka kuingiza ushoga ndani ya Kanisa yaani waoane dada kwa dada au kaka kwa kaka. Tujitahidi kujitegemea ili tusikubali mambo kama haya.

Kanisa pawe ni mahali pa watakatifu na kama hawapo wale walipo kanisani watamani kuwa watakatifu. Pasiwe ni mahali pa kutenda uovu.

Wanafunzi wa Yesu waliiwta kutoka katika tabia, kazi, hadhi na mazingira tofauti ndiyo sababu aliwaombea umoja. Nasi Mungu ametuuta tuwe katika **kundi la watakatifu** bila kujali historia.

Tukikiri na kuutumikia umoja **ulimwengu utasadiki tumetumwa na Baba**. Mkiwa kitu kimoja wanawake, wanaume, wazee, vijana na watoto **ulimwengu utasadiki**, hivyo Mungu atusaidie ili tuishi kwa umoja.

Maisha ya kanisa katika nyakati za VVU na UKIMWI

Na Mary Joel Mmbaga,
Mratibu Kitengo cha Mapambano
dhidi ya VVU na UKIMWI.

*Nitengeeni Barnaba na Sauli kwa
kazi ile niliyowaitia,” (Mdo 13: 1-3).*

Maisha ya Kanisa katika nyakati za VVU na UKIMWI yamekumbwa na changamoto nyingi sana. Kanisa kwa sasa si chombo pekee kinachotoa mafunzo kwa jamii, bali kuna taasisi nyingine zinazotoa elimu hiyo. Pia kuna vyombo vinavyoletwa na utandawazi kwa njia ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Mengi ya mafundisho haya hayana mipaka kwa umri na ufhamu wa jamii. Baadhi ya mafundisho haya yamemomonyoa si tu maadili, bali yameendelea kuipotosha jamii katika mambo yahusuyo uwakili wa Kanisa na uumbaji wa Mungu. Kanisa tumeitwa kumhudumia mwanadamu kimwili, kiakili na kiroho (*holistic approach*). Kwanza kabisa Kanisa linatakiwa kukubali kuwa tatizo lipo na limeathiri hata kazi za Kanisa. Kama tatizo lipo maana yake tunapaswa kuliangalia tatizo hili kwa mapana zaidi, kuliko kujikita pekee kwenye kinga ya magonjwa au kuzuia maambukizo mapya.

Tukumbuke kwamba watu wanaoishi na VVU wana mahitaji ambayo mengine yako nje ya huduma zetu. Haya ni pamoja na mahitaji ya kisaikolojia, kielimu, kiuchumi, kisheria na lishe. Tukumbuke pia katika kumhudumia mtu kikamilifu lazima tutambua utu, jinsi na mazingira yake.

Lazima pia tufahamu huduma yetu na matarajio ya watu wa Mungu kutoka kwetu. Watu wanapo tutazama wanatarajia nini, na je wanakipata wanachotarajia kwetu? (Isaya 40:9). Kwa mtazamo wetu Kanisa ni nani? VVU na UKIMWI vinatuhusuje sisi kama Kanisa? Tunaposema kanisa lifanye, tunamuangalia nani? Tunamwangalia Mkuu wa Kanisa, Mchungaji, Mwinjili au wahudumu wengine katika Kanisa? Kwa kuwa tumekuwa tukimwangalia ni nani wa kufanya tumejikuta tukibaki kwenye maneno tu.

Kanisa lipo ndani ya jamii, bila jamii yenye afya hakuna kanisa. Hivyo huduma zetu zinatakiwa kuanzia katika ngazi ya familia. Kwenye familia ndiko kunakoanzia Kanisa, hivyo tutakapoimarisha familia tunaimarisha Kanisa pia. Tuwezeshe Washarika kuzungumza masuala haya kulingana na mazingira waliyopo. Tunapotoa huduma tuepuke mazoea kwa kuwa na ufhamu sahihi kabla ya kutoa huduma inayohitajika.

Kwa sasa kuna maombi ya aina nyingi. Lakini pia tuijilize kuwa hivi tunafanya maombi kucombea wanaoishi na VVU ili iweje? Je tunapowaombea ni lazima wapone? Kwa sasa kumetokea waombaji wa aina nyingi, wengine wamechakachua Neno, na neno lililochakachuliwa haliwezi kumjenga mtu. Tumesikia wengine wakifufua wafu, wengine wakiponya wenye UKIMWI. Na wengine wamelazimishwa kuacha kutumia dawa za kupunguza makali ya Virusi vya UKIMWI? Je sisi kama Kanisa tunasema nini juu ya mambo



Bibi Mary Mmbaga.

haya. Luka 17:12-15 Yesu alikutana na wenye ukoma 10 aliwaambia wakajionyeshe kwa makuhani. Walipokuwa wanaenda walitakasika. mmoja wao alipoona amepona alirudi huku akimtakuza Mungu. Tunapoangalia mistari hii tunaona wazi kuwa wale walipona walitakiwa wakajionyeshe kwa makuhani. Kwa sasa tunapaswa kuwashauri wale wanaoombewa kuwa hatua ya kwanza ya kuchukua ni kwenda kwenye Vituo vya Ushauri na Upimaji wa Hiari (VCT) na kujua afya zao.

Shirika la Afya Duniani linasema: Ushauri na upimaji wa hiari ni msingi wa kufanikiwa kwa utekelezaji wa kujikinga, utunzaji na huduma zote muhimu kwa wasioishi na maambukizi na hata wale ambao tayari wanaishi na maambukizi. Tuanzie mahali sahihi. Tunapojenga nyumba tunaanza na msingi. Uimara wa nyumba unategemea sana msingi. Mahali sahihi ni kule kupata ni Ushauri na Upimaji wa hiari (VCT). Tujiulize ujumbe kuhusu ushauri na upimaji wa hiari una nafasi gani kwetu? Kubadili tabia ikiwa hujui hadhi yako ya VVU ina maana yo yote? Ukianza kwa kumwambia mtu abadilishe tabia au mwenendo haitasaidia, kama tayari ameshaambukizwa.

Tusitafute ‘mchawi,’ (Mwanzo 3: 11-13). Katika kisa hiki wahusika hawakuwa tayari kuungama bali walitafuta mtu wa kulaumu kwa kushindwa kwao.

Pengine hata sisi tunafanya hivyo. Nilishindwa kwa sababu fulani hanipi nafasi. Utetezi kuwa mambo ni mengi sana; ni wakati wa kujiliza vipaumbele vyetu ni nini hasa? Bwana Yesu anasema: “Tena mtu akinitumikia Baba atamheshimu,” (Yohana 12: 26b).

Mada hii ilitolewa wakati wa Mkutano Mkuu wa Wanawake uliofanyika Mkusa, Kibaha Julai 2014.



Baaadhi ya wajumbe wakiwa katika maandamano kabla ya kuanza Mkutano Mkuu. Picha : (c) 2014 GAZETI LA UPENDO/ EMMANUEL KIMWERI.

FAHAMU HISTORIA FUPI YA KKKT

Vyama vilivyoeneza Ulutheri

Mwanzo wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanganyika (baadaye Tanzania) kuwepo nchini ni mwaka 1887, Chama cha Misioni cha ‘Berlin III’ au ‘Evangelical Missionary Society for East Africa’ (EMS) kutoka Ujerumani kilipoanzisha kazi ya Injili Kigamboni, Dar es Salaam.

Chama cha pili

Chama cha Misioni cha ‘Berlin I’, nacho kutoka Ujerumani, kiliingia Tanzania kikitokea Afrika ya Kusini na kuanza kazi Nyanda za Juu Kusini mwaka 1891 kilipoanzisha kituo au misheni sehemu iitwayo Ipagika au Pipagika (Wangemannshöhe) katika Dayosisi ya Konde (kwa sasa).

Mwaka 1890 Chama cha Berlin III kilichukua sura mpya baada ya kubadili sera yake na kujulikana kwa jina la Bethel au Misioni ya ‘Bethel’. Misioni hii ikafika sehemu za Tanga na kuanza kazi eneo la Mbuyukenda.

Baadaye Misioni hii iliama kufikisha Injili ya Kristo nje ya mipaka ya Tanganyika. Wamisionari hao walipanga kwenda Rwanda kupitia Bukoba. Walipofika Bukoba wakafungua kituo mwaka 1910.

Chama cha Leipzig

Chama cha tatu kufika nchini Tanzania ni Chama cha Misioni cha Leipzig, nacho kutoka Ujerumani. Kiliingia nchini Tanzania mwaka 1893 na kuanza kazi ya misioni Kaskazini mwa nchi sehemu ya Kidia, Old Moshi na baada ya muda mfupi, kwa kushauriwa na Mtawala wa Kijerumani, Carl Peters, wakahamia Nkwarungo - Machame.

Pamoja na vyama vilivyoanzisha Ulutheri Tanzania, kuna mchango mkubwa wa vyama vya misioni na makanisa toka Ulaya na Marekani tunayo endelea kushirikiana nayo kama: COS, ELCB, FELM, DLM, DANMISSION, SEM, LMW, MEW, NLM, NMZ, BMW, UEM, VELKD, ELCA, nk. Hakika Neno la Mungu linaendelea kufundishwa kwa upendo na kwa usahili wakati wote huu.

Vita za Dunia

Kanisa la Kilutheri nchini lilipita katika nyakati ngumu vipindi vya Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia 1914 - 1918 na ya

Pili 1939 - 1945. Chama cha Misioni Augustana kutoka Marekani pamoja na Walutheri kutoka nchi nyingine za Ulaya walitoa msaada sana wakati wamisionari wa Kijerumani walipoondoka.

Makanisa Saba

Vyama vya misioni viliendelea na kazi ya Injili na makanisa saba ya Kilutheri yakaanzishwa maeneo mbalimbali nchini. Makanisa hayo mwaka 1948 yaliunda Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Tanganyika. Na tarehe 23 Juni 1963 makanisa yale saba yaliungana kuunda Kanisa moja la KKKT na makanisa yakageuka kuwa Dayosisi/Sinodi. Sinodi zikageuka kuwa Dayosisi na ufikapo mwezi Septemba mwaka huu KKKT itakuwa na Dayosisi 24.

Oongozi na usimamizi

Chombo kikuu cha maamuzi KKKT ni Mkutano Mkuu amba hufanyika kila baada ya miaka minne. Halmashauri Kuu ya KKKT hukutana mara mbili kwa mwaka kwa vikao vyake vya kawaida. Wajumbe wa vyombo vyote hivi wanawakilisha Dayosisi zote za KKKT.

Kazi za Umoja

Kanisa lina vituo na Ofisi Kuu ya Kazi za Umoja (Common Work). Ofisi Kuu ya Kanisa inaongozwa na Katibu Mkuu. Ina idara zifuatazo: Misioni na Uinjilisti; Mipango na Maendeleo; Fedha na Utawala; Huduma za Jamii Kazi za Wanawake na Watoto. Pia kuna Kitengo cha Ukaguzi. Kazi ya Ofisi Kuu ya KKKT ni pamoja na *kuratibisha, kuwezesha na kufanya utetezi* kwa manufaa ya Kanisa zima.

KKKT inataasisi na vituo vinavyotunza Kazi za Umoja: 1. Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira 2. Seminari Ndogo ya Kilutheri Morogoro 3. Kituo cha Redio Sauti ya Injili, Moshi. 4. Shule za Msingi kwa watoto viziwi Mwanga na Njombe. 5. Shule ya Sekondari kwa watoto viziwi Njombe. 6. Miradi ya kuongeza kipato.

Pamoja na vituo vya Kazi za Umoja, Dayosisi zina hospitali 20 na zahanati / vituo vya afya 150. Dayosisi zote zina shule za msingi, sekondari na vyuo vya ufundi na maarifa mbalimbali. Baadhi ya Dayosisi zina vyuo vikuu. Taasisi

hizi hutoa huduma kwa watu wote bila ubaguzi.

Karibu kila dayosisi /taasisi zake/ idara zina miradi midogo midogo ya kuinua kipato; miradi ya maji salama, miradi ya ng’ombe wa maziwa, nk. Dayosisi nyingi zina miradi mikubwa na ya kati. Baadhi zimeanzisha mabenki au vyama vikubwa vya kuweka na kukopa (SACCOs).

Kazi za Misioni

KKKT inajihuisha na kazi za misioni ndani na nje ya Tanzania. Baadhi ya maeneo nje ya nchi ni Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo, Msambiji, Malawi, Uganda na Zambia. Ndani ya nchi maeneo ya misioni ni Tabora, Kigoma na Zanzibar.

Ushirikiano na wengine

KKKT ni mwanachama hai wa: Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT); ‘Lutheran Mission Cooperation’ (LMC); Baraza la Makanisa Barani Afrika (AACC); Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (LWF) na Baraza la Makanisa Duniani (WCC).

Ofisi zilipo

Ofisi Kuu ya KKKT ipo Arusha “Lutheran Centre”, Barabara ya Boma mkabala na Posta Kuu. Senta hiyo ina hosteli yenye vitanda 24.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na

Katibu Mkuu

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania

S.L.P. 3033, Arusha

Simu: 250 8856/ 250 8857

Fax 254 8858

Barua pepe: elcthq@elct.or.tz

Tovuti: <http://www.elct.org/>

Au: <http://www.elct.or.tz/>

Walutheri wafika milioni 6.3 Tanzania

Katibu Mkuu wa KKKT, Bw. Brighton Killewa, alitangazahivi karibuni takwimu za wanachama wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania kwamba wakristo 201,225 waliongezekwa mwaka jana ukilinganisha na mwaka uliotangulia, hivyo kufanya idadi ya walutheri kufikia 6,341,103 ikilinganishwa na 6,139,878 mwaka 2012.

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania

VITABU NA MAANDIKO



Jipatie nakala ya vitabu hivi na maandiko mengine ya Dini toka Dayosisi yako au wasiliana na:

Idara ya Misioni na Uinjilisti KKKT

S.L.P. 3033

ARUSHA

Barua pepe: elcthq@elct.or.tz